



Home Office

Jukumu la wataalamu wa afya na huduma za kijamii na walimu kuripoti ukeketaji wa wanawake (FGM) kwa polisi

Jukumu hilo ni lipi?

Mnamo tarehe 31 Oktoba 2015, jukumu lilianzishwa ambalo linahitaji wataalamu wa afya na huduma za kijamii na walimu kuripoti polisi kesi za ukeketaji (FGM) 'zinazojulikana' kwa wasichana wenye umri ulio chini ya miaka 18.

Kwa mfano, kama daktari anaona kwamba msichana mwenye umri ulio chini ya miaka 18 amekeketwa, atahitaji kupiga ripoti kwa polisi. Au, kama msichana atamwambia mwalimu ya kwamba amekeketwa, mwalimu atahitajika kuripoti jambo hili kwa polisi.

Ni nini kitafanyika baada ya kesi kuripotiwa kwa polisi?

Ukeketaji (FGM) ni uhalifu mkubwa na polisi watahitajika kuchunguza kila kesi ambayo imeripotiwa ipasavyo.

Polisi watafanya kazi pamoja na wataalamu wa huduma za jamii kuhakikisha kwamba msichana yuko salama na mahitaji yake yamepewa kipau mbele.

Kwa nini jukumu hili limeanzishwa?

Wakati msichana amepitia ukeketaji, uhalifu mkubwa umetokea kwa hivyo kuna umuhimu mkubwa kwamba polisi wamehusishwa haraka iwezekanavyo. Hii itahakikisha kwamba uchunguzi sahihi umefanyika.

Madhumuni ya jukumu hili ni kusaidia kuhakikisha kwamba wataalamu wana imani ya kukabiliana na ukeketaji na kusaidia kuongeza idadi ya kesi zinazorejeshwa kwa polisi ili kesi hizo zichunguzwe ipasavyo.

Nini jukumu hili halitafanya

Halimaanishi kwamba polisi watachukua hatua bila kushauriana ipasavyo na wataalamu wa huduma za jamii na wataalamu wengine wanaohusika.

Halitahitaji wataalamu kuripoti kesi kwa polisi ambazo *wanatuhumu* kwamba ukeketaji unaweza kuwa umefanyika au ambazo wanafikiria kuwa msichana *anaweza kuwa hatarini*. Jukumu hili halihusu wanawake wenye umri wa miaka 18 au zaidi. Wataalamu watafuata utaratibu wa ulindaji uliopo kuhusu kesi hizi.

Mukhtasari: Lazima kuripoti ukeketaji (FGM)*

Jukumu hili linahusisha wataalamu wa afya waliojiandikisha na wataalamu wa huduma za jamii na walimu katika Uingereza na Wales.

Linahitaji wataalamu hawa kuripoti kwa polisi, katika utekelezajii wa majukumu yao, kama:

- Wamepokea taarifa kutoka kwa msichana aliye chini ya umri wa miaka 18 kwamba kitendo cha ukeketaji kimefanyika kwake; au
- Wameona ishara za kimwili zinazoonyesha kwamba kitendo cha ukeketaji kimefanywa kwa msichana aliye chini ya umri wa miaka 18 na kuwa hakuna sababu ya kuamini kwamba kitendo hiki kilikuwa muhimu kwa afya ya kimwili au kiakili ya msichana au kwa madhumuni yanayohusika na uzazi.

*Lilianzishwa katika Sehemu ya 5B ya Sheria ya Ukeketaji 2003, na kuingizwa kwa kufungu cha 74 cha Sheria ya Uhalifu Mkuu 2015